JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (VIKUNDI VYA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA VYA KIJAMII) LA MWAKA 2019

[SHERIA NDOGO]

Toleo hili la Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Vikundi vya Huduma Ndogo za Fedha vya Kijamii) la Mwaka 2019, ni Tafsiri Rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

Dodoma,
……………., 2020

ADELARDUS L. KILANGI
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

TANGAZO LA SERIKALI Na. 678 Lililochapishwa 13/9/2019

SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA
(SURA YA 407)

________

KANUNI

________

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 60(1) na (2))*

__________

KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (VIKUNDI VYA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA VYA KIJAMII), 2019

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UUNDAJI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

4. Uanzishaji wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.
5. Mkutano wa awali.
6. Kamati ya Muda na majukumu yake.
7. Mkutano wa uanzishaji na majukumu yake.

SEHEMU YA TATU
USAJILI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

8. Maombi ya usajili.
9. Jina la kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.
10. Maamuzi ya maombi ya usajili.
11. Hati ya usajili.

12. Kikao cha kwanza.
13. Kukataliwa kwa usajili.
14. Maombi rejea ya usajili.
15. Rufaa kwa kukataliwa usajili.
16. Rejesta ya vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii.
17. Kufutwa kwa usajili.

SEHEMU YA NNE
UENDESHAJI

18. Kuanza shughuli za uendeshaji.
19. Shughuli zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa.
20. Masharti ya uendeshaji.
21. Uwasilishaji wa taarifa.
22. Utawala wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.
23. Kumlinda mlaji.
24. Ushirikiano na taasisi nyingine.

SEHEMU YA TANO
UFUATILIAJI NA UDHIBITI WA NDANI

25. Ufuatiliaji.
26. Uteuzi wa mdhibiti wa ndani.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

27. Ubadilishanaji wa taarifa za mikopo.
28. Kumtumia mhamasishaji.
29. Kipindi cha mpito.
30. Kuhama daraja kwa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.
31. Adhabu za jumla.
32. Hatua za kiutawala.

---

MAJEDWALI

---

TANGAZO LA SERIKALI Na. 678 Lililochapishwa 13/9/2019

SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA,
(SURA YA 407)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 60 (1) na (2))*

KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (VIKUNDI VYA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA VYA KIJAMII), 2019

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Vikundi vya Huduma Ndogo za Fedha vya Kijamii) za Mwaka 2019.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa watoa huduma ndogo za fedha waliosajiliwa kutoa huduma katika Daraja la 4 kwa mujibu wa Sheria.

Tafsiri

3. Katika kanuni hizi, isipokuwa muktadha ukihitaji vinginevyo-

"Akaunti" maana yake ni akaunti ya benki au fedha za kielektroniki;

Sheria Na. 10 ya Mwaka 2018

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha;

"afisa aliyeidhinishwa" maana yake ni mtu ambaye ameteuliwa katika nafasi hiyo na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

Sura 197

"Benki" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania;

"kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"katiba" maana yake ni makubaliano ya maandishi

yaliyopitishwa na kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kwa mujibu wa Kanuni hizi;

Sura. 287 na 288

"taasisi ya ubadilishanaji wa taarifa za mikopo" maana yake ni taasisi mahsusi inayokusanya na kuuza taarifa za mikopo za watu binafsi na taasisi;

"Mamlaka Kasimishwa" maana yake ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyokasimishwa na Benki kutekeleza majukumu na kuwa na mamlaka ya Benki kuhusiana na vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii kwa mujibu wa Sheria;

"mkopo mdogo wa nyumba" maana yake ni mkopo usiyo na dhamana au wenye dhamana unaotolewa kwa kaya zilizopo maeneo ya vijijini au mjini ili kujenga au kukarabati au kuboresha nyumba;

"wanachama wa awali" maana yake ni wanachama waliohusika kuanzisha kikundi;

"Mamlaka ya Serikali za Mitaa" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"mwanachama" maana yake ni mtu ambaye ni mwanachama kwa mujibu wa katiba ya kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichosajiliwa;

"mtoa huduma ndogo za fedha" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha;

"mhamasishaji" maana yake ni mtu binafsi au taasisi iliyosajiliwa kwa ajili ya kuhamasisha na kuwezesha biashara ya huduma ndogo za fedha ikijumuisha uanzishaji, usajili na uendeshaji wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii;

"michango" maana yake ni makusanyo ya fedha yaliyokubaliwa na wanachama wa kikundi ili kupata mtaji wa kikundi;

"Daraja la 4" maana yake ni aina ya watoa huduma ndogo za fedha inayojumuisha kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHAJI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

Uanzishaji wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii

4.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinaweza kuanzishwa na watu binafsi walioungana kwa lengo la kuendesha biashara ya huduma ndogo za fedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinaweza kuanzishwa na idadi ya watu kumi hadi hamsini walio na malengo yanayowiana kwa ajili ya shughuli za kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

Mkutano wa awali

5.-(1) Watu ambao wanakusudia kuanzisha kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii wataitisha mkutano wa awali kwa madhumuni ya -

(a) kujadili na kukubaliana kuhusu uanzishwaji, malengo na katiba ya kikundi; na

(b) kuchagua kamati ya muda kwa ajili ya kuwezesha uanzishwaji wa kikundi.

(2) Wajumbe wa mkutano wa awali watachukuliwa kuwa ni wanachama wa awali wa kikundi tarajiwa cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

Kamati ya Muda na majukumu yake

6.-(1) Kamati ya muda iliyochaguliwa chini ya kanuni ya 5 itakuwa na idadi ya wajumbe kama itakavyoamuliwa kwenye mkutano wa awali.

(2) Majukumu ya kamati ya muda yatakuwa yafuatayo-

(a) kupendekeza jina na malengo ya kikundi kinachoanzishwa;

(b) kuandaa rasimu ya katiba ya kikundi ambayo, kwa kiwango cha chini itajumuisha masuala yaliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi;

(c) kuorodhesha majina ya wanachama wa awali

na kuchukua taarifa za mkutano wa awali;
(d) kupendekeza muundo wa kikundi;
(e) kuandaa au kupata nyaraka zote muhimu kwa madhumuni ya kutimiza vigezo vya usajili;
(f) kufanya mkutano wa uanzishwaji wa kikundi; na
(g) kufanya mkutano wa kwanza baada ya usajili wa kikundi.

Mkutano wa Uanzishaji na majukumu yake

7.-(1) Kutakuwa na mkutano wa uanzishaji wa kikundi wa wanachama wa awali ambao utaandaliwa na kamati ya muda kwa madhumuni ya kuanzisha na kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii.

(2) Mkutano wa uanzishaji utakaofanywa chini ya kanuni ndogo ya (1) unaweza kufanywa chini ya uongozi wa afisa aliyeidhinishwa au mhamasishaji na utakuwa na majukumu yafuatayo-
(a) kupitisha jina na malengo ya kikundi yaliyopendekezwa;
(b) kukubaliana kuhusu muundo wa kikundi kama ulivyopendekezwa na kamati ya muda;
(c) kupendekeza majina ya viongozi wa kikundi;
(d) kujadili na kuthibitisha rasimu ya katiba na nyaraka zingine zilizoandaliwa na kamati ya muda kwa madhumuni ya kuomba usajili wa kikundi; na
(e) kuipatia kamati ya muda jukumu la kukamilisha nyaraka muhimu kwa ajili ya usajili na kuziwasilisha Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(3) Endapo wanachama wa awali au kamati ya muda imemhusisha mhamasishaji kwa madhumuni ya kusaidia uanzishwaji na usajili wa kikundi, majukumu ya mhamasishaji yatajumuisha-
(a) kuandaa katiba na nyaraka zingine muhimu kwa ajili ya uanzishaji na usajili wa

kikundi;

(b) kutoa mafunzo kwa wanachama wa awali ili kuwezesha mchakato wa uanzishaji na usajili; na

(c) kutekeleza kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na wanachama wa awali au kamati ya muda kwa madhumuni ya uanzishaji na usajili wa kikundi.

(4) Majukumu ya mhamasishaji kwa madhumuni ya uanzishaji na usajili wa kikundi yatakoma mara tu usajili wa kikundi utakapokamilika; isipokuwa kama atahitajika kufanya shughuli zingine za uhamasishaji.

## SEHEMU YA TATU
## USAJILI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

Maombi ya usajili

8.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho kinakusudia kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha kitatuma maombi ya usajili kwa Benki au kwa Mamlaka Kasimishwa kwa kutumia Fomu Na. 2 iliyoanishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(2) Maombi yaliyofanywa chini ya kanuni ndogo ya (1) yataambatishwa na vifuatavyo-

(a) nakala mbili za katiba zilizosainiwa na wanachama wote;

(b) nakala mbili za mihtasari ya mikutano ya uanzishaji ambayo imesainiwa na wanachama wote;

(c) maazimio ya wanachama kuanzisha na kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii yatakayowasilishwa kupitia Fomu Na. 1 kama ilivyoanishwa katika Jedwali la Pili;

(d) mapendekezo ya muundo wa kikundi na majina ya viongozi wanaopendekezwa na mwombaji;

(e) orodha ya wanachama, kwa kuzingatia

kwamba idadi ya wanachama inakidhi kanuni ya 4(2);
(f) uthibitisho wa malipo ya michango ya wanachama wa awali;
(g) barua ya utambulisho wa mwombaji kutoka mamlaka ya kata au ya kijiji; na
(h) nyaraka au taarifa nyingine yoyote muhimu.

Jina la kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii

9.-(1) Jina la kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii lililopendekezwa kwa madhumuni ya maombi ya usajili litakuwa la kipekee na litajumuisha maneno "Kikundi cha Huduma Ndogo za Fedha cha Kijamii".

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) jina la kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii halitajumuisha neno "benki".

Maamuzi ya maombi ya usajili

10.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa itapaswa, ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea nyaraka za maombi ya usajili zilizokamilika, kufanyia kazi maombi na kutoa maamuzi.

(2) Pale ambapo Benki au Mamlaka Kasimishwa imepokea nyaraka ambazo hazijakamilika au zenye makosa kwa madhumuni ya usajili, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza, kabla ya kuamua maombi hayo, kumtaka mwombaji-
(a) kuwasilisha nyaraka au taarifa zilizokosekana; au
(b) kurekebisha makosa hayo ili kukidhi vigezo vya usajili.

Hati ya usajili

11.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa, baada ya kujiridhisha kwamba vigezo vyote vimekamilika, itasajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii na kukipatia hati ya usajili;

(2) Endapo Benki au Mamlaka Kasimishwa haijaridhika na utekelezaji wa masharti ya maombi, itakataa maombi ya usajili.

(3) Hati ya usajili iliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) itakuwa kwenye Fomu Na. 3 kama

ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(4) Hati ya usajili iliyotolewa chini ya Kanuni hizi itaanza kutumika kuanzia tarehe iliyotolewa na itaendelea kuwa halali hadi itakapofutwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Kikao cha kwanza

12.-(1) Kamati ya muda itaitisha kikao cha kwanza, ndani ya mwezi mmoja tangu kupokea hati ya usajili, kwa madhumuni ya-

(a) kuwasilisha hati ya usajili kwa wanachama wa kikundi;
(b) kuthibitisha viongozi waliopendekezwa au kuchagua viongozi wa kikundi kwa mujibu wa katiba;
(c) kuvunja kamati ya muda; na
(d) kujadili masuala mengine kama wanachama watakavyoona inafaa au kama ilivyoainishwa kwenye katiba.

(2) Katika kikao cha kwanza, hakuna kanuni yoyote itakayomzuia mjumbe wa kamati ya muda kuchaguliwa kuwa kiongozi wa kikundi.

Kukataliwa kwa usajili

13.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kukataa kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii pale ambapo kikundi hicho kimeshindwa kufanya yafuatayo-

(a) kukidhi masharti ya maombi ya usajili kama yalivyoainishwa kwenye kanuni ya 8 ya Kanuni hizi; au
(b) kuwasilisha taarifa au nyaraka sahihi na stahiki zinazohitajika kwa ajili ya usajili.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Kasimishwa imekataa kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii, ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya maamuzi hayo, itatoa notisi ya maandishi kwa kikundi ikielezea sababu za kukataa.

Maombi rejea ya usajili

14. Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho maombi yake ya usajili yamekataliwa chini ya kanuni ya 13 kinaweza kuwasilisha maombi

mapya baada ya kukamilisha mapungufu yaliyoonekana wakati wa maombi ya awali au mapitio yaliyofuata yamerekebishwa au kushughulikiwa vinginevyo.

Rufaa kwa kukataliwa usajili

15.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho hakijaridhishwa na maamuzi ya Benki au Mamlaka Kasimishwa chini ya kanuni ya 13 kinaweza, ndani ya siku thelathini, kuanzia tarehe ya kupokea notisi ya maandishi-

(a) ikiwa ni maamuzi ya Mamlaka Kasimishwa, kukata rufaa kwa Benki; au
(b) ikiwa ni maamuzi ya Benki, kukata rufaa kwa Waziri.

(2) Rufaa iliyokatwa chini ya kanuni ndogo ya (1), itakuwa ya maandishi na itaelezea kwa uwazi yafuatayo-

(a) kiini cha rufaa;
(b) sababu za rufaa; na
(c) masuala mengine yoyote muhimu.

(3) Waziri ataamua rufaa kwa mujibu ya masharti ya Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (Majukumu ya Waziri), 2019.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), Benki au Waziri, ndani ya siku sitini tangu tarehe ya kupokea maombi ya rufaa, ataamua rufaa hiyo.

(5) Katika kuamua rufaa chini ya kanuni ndogo ya (3), Benki au Waziri anaweza kumtaka mkata rufaa kuwasilisha nyaraka au taarifa zozote muhimu ambazo zinajenga msingi wa rufaa yake.

Rejesta ya vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii

16.-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 54 cha Sheria, Benki au Mamlaka Kasimishwa itaweka na kutunza rejesta ya vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii.

(2) Rejesta inayotajwa katika kanuni ndogo ya (1) itakuwa na taarifa zifuatazo-

(a) jina, anuani na mawasiliano ya kikundi;
(b) majina na mawasiliano ya viongozi wa kikundi;
(c) eneo la kutoa huduma;

(d) namba ya usajili;
(e) tarehe ya usajili;
(f) idadi ya wanachama; na
(g) taarifa nyingine yoyote ambayo Benki au Mamlaka Kasimishwa itaona inafaa.

Kufutwa kwa usajili

17.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa, pale itakapojiridhisha kwamba kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichosajiliwa kimeshindwa kutekeleza vigezo na masharti ya usajili, au kimekiuka masharti ya Sheria au Kanuni hizi, inaweza kufuta hati ya usajili na kuondoa jina la kikundi katika rejesta.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Kasimishwa imefuta usajili wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii, itakipatia kikundi notisi ya maandishi ambayo pamoja na mambo mengine, itaelezea sababu za maamuzi hayo.

(3) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ambacho hakijaridhishwa na maamuzi ya Benki au Mamlaka Kasimishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) kinaweza, ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kupokea notisi ya maandishi-

(a) ikiwa ni maamuzi ya Mamlaka Kasimishwa, kukata rufaa kwa Benki; au
(b) ikiwa ni maamuzi ya Benki, kukata rufaa kwa Waziri.

(4) Masharti ya kanuni ya 15 yanayohusiana na rufaa yatatumika kama yalivyo pamoja na marekebisho madogo stahiki.

## SEHEMU YA NNE
## UENDESHAJI

Kuanza shughuli za uendeshaji

18.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichosajiliwa kitaanza kujiendesha ndani ya miezi mitatu kuanzia tarehe ya usajili.

(2) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza, kwa notisi ya maandishi ya siku kumi na nne, kufuta usajili wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii chochote ambacho kimeshindwa kuanza

kujiendesha kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1).

(3) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichosajiliwa ambacho hakijaridhika na maamuzi ya Benki au Mamlaka Kasimishwa chini ya kanuni ndogo ya (2) kinaweza, ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kupokea notisi ya maandishi-

(a) ikiwa ni maamuzi ya Mamlaka Kasimishwa, kukata rufaa kwa Benki; au

(b) ikiwa ni maamuzi ya Benki, kukata rufaa kwa Waziri.

(4) Masharti ya kanuni ya 15 yanayohusiana na rufaa yatatumika kama yalivyo pamoja na marekebisho yoyote madogo stahiki.

Shughuli zinazoruhusiwa na zisizoruhusiwa

19.-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 36 cha Sheria, shughuli zinazoruhusiwa kufanywa na kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii zitajumuisha yafuatayo:

(a) kuhamasisha ukusanyaji wa michango kutoka kwa wanachama wake;

(b) kutoa mikopo kwa wanachama wake;

(c) kuhamasisha ukusanyaji fedha kwa ajili ya ustawi wa kijamii na kiuchumi kwa wanachama wake; na

(d) shughuli zingine zozote zitakazoidhinishwa na Benki.

(2) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii hakitaruhusiwa kufanya shughuli zifuatazo-

(a) kupokea akiba kutoka kwa wasio wanachama;

(b) kufungua tawi, wakala au kituo cha huduma; au

(c) shughuli zingine zozote kama zitakavyoainishwa na Benki.

Masharti ya uendeshaji

20.-(1) Bila kujali masharti yoyote katika Kanuni hizi yanayomaanisha vinginevyo, kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kilichosajiliwa kitapaswa-

(a) kuwa na anuani ya mahali au eneo

wanalokutana kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha;

(b) kuendesha biashara ya huduma ndogo ya fedha kwa mujibu wa Sheria, Kanuni hizi na katiba ya kikundi;

(c) kufungua na kuendesha akaunti ya benki au taasisi yoyote ya fedha au aina yoyote ya akaunti kwa ajili ya kuendesha shughuli zake;

(d) kuwajibika kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa;

(e) kugawa faida au kulipa riba kwa wanachama wake kwa mujibu wa katiba yake;

(f) kuweka na kutunza taarifa za kumbukumbu za msingi za fedha na taarifa zingine muhimu zinazohusu uendeshaji wake;

(g) kuwezesha hesabu na kumbukumbu za fedha kufuatiliwa au kukaguliwa kama ilivyoanishwa kwenye Kanuni hizi;

(h) kuweka na kutunza mihtasari ya mikutano, rejesta ya wanachama, nakala za katiba na kumbukumbu zingine muhimu;

(i) kuteua mtu atakayewajibika na udhibiti wa ndani wa masuala ya fedha kama ilivyoainishwa katika Kanuni;

(j) kuwasilisha taarifa na masuala mengine muhimu kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi; na

(k) kuzingatia misingi ya kumlinda mtumiaji kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi.

(2) Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kutoa waraka na miongozo kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa masharti ya uendeshaji kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1).

Uwasilishaji wa taarifa

21.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kwa kila robo mwaka, kitawasilisha taarifa za kumbukumbu za msingi za fedha na masuala mengine

muhimu kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa.

(2) Taarifa zinazorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) zitawasilishwa kwa namna iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu na kwa kiwango cha chini zitajumuisha yafuatayo-

(a) michango ya wanachama, michango iliyohamasishwa, orodha ya mikopo, matumizi, mapato, mgawanyo wa ziada na mikopo ya kikundi;
(b) kumbukumbu za idadi, mahudhurio na masuala husika ya mikutano iliyofanyika ndani ya robo mwaka; na
(c) taarifa zingine muhimu kama zitakavyoweza kuainishwa na Benki au Mamlaka Kasimishwa.

Utawala wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii

22.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitahakikisha masuala yote yanayohusu utawala wa kikundi yameainishwa katika katiba yake.

(2) Kwa dhumuni la kuwa na utawala bora, kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitahakikisha-

(a) kinaitisha mikutano ikiwemo mikutano ya kawaida na mikutano mikuu kwa namna ilivyoainishwa katika katiba yake;
(b) kinachagua kidemokrasia viongozi wenye uadilifu kwa mujibu wa katiba yake;
(c) kuna uwazi na uwajibikaji wa masuala yake kwa wanachama wake; na
(d) kinatekeleza shughuli nyingine yoyote kwa madhumuni ya kuhakikisha kuna utawala bora.

Kumlinda mlaji

23. Kwa madhumuni ya kuzingatia misingi ya kumlinda mlaji, kila kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitapaswa-

(a) kuwa na taratibu za kushughulikia malalamiko na kutatua migogoro na kuteua mtu au watu kutoka miongoni mwa wanachama watakaoshughulikia malalamiko

na migogoro ya wanachama, ndani ya katiba yake;

(b) kuwa na mfumo wa kutoa elimu ya kifedha kwa wanachama wake;

(c) kuhakikisha kwamba vigezo na masharti ya mikopo au huduma zinazohusu mikopo ni ya wazi, haki, yanakubalika na yanalinda haki za wanachama;

(d) kuweka wazi kwa wanachama taarifa zinazohusu mwenendo wa kikundi;

(e) kuhakikisha kwamba kila mwanachama wa kikundi anaielewa katiba na anapewa nakala ya katiba;

(f) kuhakikisha kwamba taratibu za kukusanya na kurejesha madeni zinalinda haki za wanachama; na

(g) kufanya shughuli nyingine yoyote inayokusudiwa kulinda haki na maslahi ya wanachama wake.

Ushirikiano na taasisi nyingine

24.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinaweza kushirikiana na taasisi zingine kwa madhumuni ya uendeshaji bora wa shughuli zake ikiwemo upatikanaji wa-

(a) huduma za kifedha kutoka benki na taasisi za fedha ikiwa ni pamoja na mikopo na akaunti za benki;

(b) misaada ya kifedha kutoka kwa asasi au taasisi zisizo za kifedha; na

(c) elimu ya fedha na huduma zingine za uwezeshaji kutoka kwa asasi au taasisi husika.

(2) Endapo kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinakusudia kupata mkopo kutoka kwa benki, taasisi ya fedha au taasisi nyingine yoyote, kitahakikisha kwamba-

(a) vigezo na masharti ya mkopo ni ya wazi na yanakubalika na wanachama wote wa kikundi; na

(b) mkopo hautazidi jumla ya mali za kikundi

isipokuwa kama mkopo huo una dhamana ambayo inaweza kufidia mkopo wote.

(3) Endapo kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinapokea huduma ya kifedha kutoka benki, taasisi ya kifedha au taasisi nyingine yoyote inayotoa huduma ndogo za fedha kidigitali, kitahakikisha wanachama wake wana uelewa wa kutosha wa huduma inayotolewa ikiwemo vihatarishi, gharama na faida.

## SEHEMU YA TANO
## UFUATILIAJI NA UDHIBITI WA NDANI

Ufuatiliaji

25.-(1) Benki au Mamlaka Kasimishwa itafanya ufuatiliaji endelevu wa uendeshaji wa vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii.

(2) Benki au Mamlaka Kasimishwa, kwa madhumuni ya ufuatiliaji wa uendeshaji wa kikundi, itatekeleza wajibu ufuatao-

(a) kupitia na kuchambua taarifa husika zilizowasilishwa na kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii;

(b) kupitia na kuchambua malalamiko na migogoro iliyowasilishwa kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa kwa madhumuni ya kuyapatia ufumbuzi;

(c) kuvitembelea rasmi vikundi vya huduma ndogo za fedha vya kijamii ili kubaini utendaji kazi wake na uzingatiaji wa masharti ya Sheria na Kanuni hizi; na

(d) kutekeleza majukumu yoyote kama itakavyoona inafaa.

(3) Endapo Benki au Mamlaka Kasimishwa, katika kutekeleza majukumu yake chini ya kanuni ndogo ya (2) itabaini mapungufu, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza, kwa maandishi kutoa ushauri au kukielekeza kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii, kurekebisha mapungufu hayo ndani ya siku ishirini na moja au kwa kipindi ambacho Benki au Mamlaka Kasimishwa itaona kinafaa.

Uteuzi wa mdhibiti wa ndani

26.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii, kupitia mkutano rasmi, kitateua mtu miongoni mwa wanachama au nje ya wanachama ambaye atakuwa na jukumu la udhibiti wa ndani wa masuala ya kifedha na uendeshaji.

(2) Mtu aliyeteuliwa chini ya kanuni ndogo ya (1) atapaswa kuwa mtu mwenye uadilifu na ambaye ana angalau cheti cha elimu ya sekondari na atakuwa na majukumu yafuatayo-

(a) kukagua na kupitia nyaraka zote husika ikijumuisha kumbukumbu za fedha, rejesta ya wanachama, fomu za mikopo na mihtasari ya mikutano ili kuhakikisha utekelezaji;

(b) kuandaa taarifa ya nyaraka zilizokaguliwa au kupitiwa na kuwasilisha taarifa kwa wanachama;

(c) kuhakikisha matokeo na mapendekezo yanayolenga kuboresha uendeshaji wa kikundi yametekelezwa ipasavyo;

(d) kuhakikisha kwamba ushauri, amri au maelekezo yaliyotolewa na Benki au Mamlaka Kasimishwa yametekelezwa ipasavyo;

(e) kuhakikisha nyaraka na taarifa zote ni sahihi na zinawasilishwa kwa Benki au Mamlaka Kasimishwa kwa wakati;

(f) kuhakikisha kwamba kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kimefuata masharti yote ya uendeshaji yalioainishwa chini ya kanuni ya 20;

(g) kuhakikisha kuwa uendeshaji wa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii ikijumuisha uhamasishaji wa michango ya wanachama, michango, utoaji wa mikopo na mgawanyo wa ziada unazingatia masharti ya Sheria, Kanuni hizi na katiba;

(h) kuhakikisha kwamba kuna mgawanyo wa majukumu na wajibu miongoni mwa viongozi na wanachama; na

(i) kutekeleza majukumu mengine yoyote kama atakavyoelekezwa na wanachama au kwa mujibu wa katiba.

(3) Mtu atakayeteuliwa chini ya kanuni ndogo ya (1)-

(a) hatajihusisha na uendeshaji wa kikundi kama vile kuidhinisha mikopo, kuandaa kumbukumbu, kupokea michango na kutunza fedha za kikundi;

(b) atahakikisha kwamba hakuna mgongano wa kimaslahi unaohusu majukumu yake ya uendeshaji au shughuli za kikundi; na

(c) hatachaguliwa au kuteuliwa kuwa kiongozi wa kikundi wakati akitekeleza majukumu yake.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA JUMLA

Ubadilishanaji wa taarifa za mikopo

27.-(1) Kila kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitaweka na kutunza taarifa za mikopo za wanachama wake kwa madhumuni ya kubadilishana taarifa kupitia taasisi ya ubadilishanaji wa taarifa za mikopo.

(2) Taarifa ya mikopo chini ya kanuni hii itawasilishwa kwa taasisi ya ubadilishanaji wa taarifa za mikopo na kubadilishana kwa namna ambavyo itaelekezwa na Benki na kwa mujibu wa masharti ya Sheria na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania. (Sura ya 197)

(3) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitahakikisha kwamba wanachama wote wameridhia kwa maandishi kuruhusu kikundi kupata, kubadilishana au kuweka wazi taarifa zote za mikopo zinazohusu wanachama kwa wakopeshaji au taasisi ya ubadilishanaji wa taarifa za mikopo.

(4) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "taarifa za mikopo" maana yake ni taarifa zozote zikijumuisha taarifa zinazohusu utambulisho wa mtu, jina kamili, tarehe ya kuzaliwa, eneo la makazi, maeneo ya makazi ya awali, hali ya ndoa, jina la mwenza, sehemu ya kazi,

sehemu za awali za kazi, mwenendo wa ulipaji, madeni yaliyopo, mali na maulizo ya historia ya mikopo au taarifa zinazohusu taasisi au biashara ambazo zitasaidia kutambua taasisi au taarifa za biashara zinazohusu usajili, kodi, wakurugenzi, utawala, madeni yaliyopo, mali, maulizo ya historia ya madeni na taarifa zingine za biashara.

Kumtumia mhamasishaji

28.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinaweza kumtumia mhamasishaji kwa madhumuni ya kuhamasisha shughuli za kikundi na kikundi kitahakikisha kwamba mhamasishaji amesajiliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha (Majukumu ya Waziri).

(2) Mhamasishaji atakayetumiwa chini ya kanuni ndogo ya (1) hatokuwa na haki za kipekee za kutoa huduma za uhamasishaji kwa kikundi.

Kipindi cha mpito

29.-(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 57 cha Sheria, kikundi kilichokuwa kinaendesha biashara ya huduma ndogo za fedha kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria na ambacho kinashindwa kutimiza masharti ya usajili ndani ya muda wa miezi kumi na mbili baada ya kuanza kutumika kwa Sheria kitafunga biashara na kukoma kuendesha biashara ya huduma ndogo za fedha.

(2) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria.

Kuhama daraja kwa kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii

30.-(1) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinaweza, kwa kutuma maombi na kufikia vigezo vilivyoainishwa kwenye kanuni husika zilizoandaliwa chini ya Sheria au sheria nyingine yoyote, kwenda Daraja lingine.

(2) Kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii hakiwezi kuomba kuhamia daraja lingine kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) isipokuwa-

(a) kikundi hicho, kwa maandishi, kimeijulisha

Benki au Mamlaka Kasimishwa nia ya kuhama kwake; na

(b) wanachama wake wameamua kuhama kwa mujibu wa katiba ya kikundi.

Adhabu za jumla

31. Mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Kanuni hizi, pale ambapo adhabu haijaainishwa atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia, atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Hatua za kiutawala

32.-(1) Bila kuathiri adhabu zilizowekwa kwenye Sheria, pale ambapo kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kimeshindwa kutekeleza masharti ya Sheria au Kanuni hizi, Benki au Mamlaka Kasimishwa inaweza kuchukua hatua za kiutawala kama itakavyoona inafaa kuhakikisha utekelezwaji wa masharti hayo.

(2) Hatua za kiutawala zilizorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) zitajumuisha yafuatayo-

(a) kusimamisha mgao wa ziada au faida unaofanywa kwa wanachama;

(b) kusimamisha au kufuta usajili;

(c) kuwasimamisha viongozi kutekeleza majukumu yao pale ambapo viongozi hao wamevunja masharti ya Sheria, Kanuni hizi au sheria nyingine yoyote;

(d) kutoa onyo au amri ikikielekeza kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kurekebisha mapungufu; na

(e) hatua nyingine yoyote inayokusudia kuhakikisha kuna utekelezaji wa Sheria na Kanuni hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limeandaliwa chini ya kanuni ya 6(2)(b))*

MFANO WA KATIBA YA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

Kwa mujibu wa kanuni ya 6 (2), katiba ya kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kwa kiwango cha chini itajumuisha yafuatayo:

1 Jina, anuani ya mahali na mawasiliano

2 Sehemu ya biashara na eneo la uendeshaji

3 Malengo ya kikundi

4 Masuala ya uanachama yakijumuisha, michango ya uanachama, michango ya vipindi, kukubaliwa, haki, wajibu, kusimamishwa na kufutwa uanachama;

5 Masuala ya utawala yakijumuisha uongozi, muda, uchaguzi, majukumu ya viongozi, kufutwa na kusimamishwa kwa viongozi;

6 Mikutano ikijumuisha ya Kawaida, Maalum na Mikutano ya Mwaka;

7 Taratibu za mkutano zikijumuisha notisi, ajenda, akidi, mihtasari na maazimio;

8 Masuala ya uendeshaji yakijumuisha michango ya wanachama, shughuli zinazoruhusiwa kufanywa, taratibu za kuhamasisha ukusanyaji wa fedha na utoaji wa mikopo;

9 Mgawanyo wa ziada;

10 Taarifa na utunzaji kumbukumbu zikijumuisha kuweka wazi taarifa za fedha na taarifa kwa wanachama na mamlaka husika kwa madhumuni ya uwazi;

11 Utaratibu wa kushughulikia malalamiko na migogoro kwa madhumuni ya kutatua migogoro;

12 Uvunjaji wa kikundi ikiwemo sababu na taratibu ; na

13 Mapitio na marekebisho ya katiba.

Fomu Na.1

JEDWALI LA PILI

AZIMIO LA KUANZISHA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

*(Imeandaliwa chini ya kanuni ya 8(2)(c))*

Sisi tulioweka saini kwenye mkutano uliofanyika tarehe …………………. mahali ……………… tumekubaliana na kuamua kuanzisha kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kitachojulikana kwa jina la KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII CHA *(Jina la Kikundi)* ……………………………………………………….

| | JINA LA MWANAKIKUNDI | SAINI |
|---|---|---|
| 1. | ……………………….……………….. | …………………..……..…… |
| 2. | ………………………….………….…. | …………………………….. |
| 3. | ………………….…………………….. | …………………………….. |
| 4. | ……………………………………….. | ……………………………… |
| 5. | ………………………………………. | ………………………………. |
| 6. | ………………………………………. | ………………………………. |
| 7. | ……………………………………….. | ……………………………….. |
| 8. | ……………………………………….. | ……………………………….. |
| 9. | ………………………………………. | ……………………………….. |
| 10. | …………………………………. | …………………………………. |

Fomu Na.2

MAOMBI YA USAJILI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII

*(Imeandaliwa chini ya kanuni ya 8(1))*

KWA: GAVANA

BENKI KUU YA TANZANIA

S. L. P …………………………….

……..…………………………………..

AU

KWA: MAMLAKA KASIMISHWA

S.L. P ……………………….

…………………………………..

YAH: MAOMBI YA USAJILI WA KIKUNDI CHA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA CHA KIJAMII CHA ……..………..………….............(*Jina la kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii*)

1. Sisi tulioweka saini, kwa niaba ya kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii kinachopendekezwa, tunaomba usajili wa kikundi tajwa hapo juu chini ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, 2018.

2. Kwa mujibu wa kanuni ya 8(2), tunaambatisha maombi yetu pamoja na vifuatavyo:

(a) nakala mbili za katiba zilizosainiwa na wanachama wote;

(b) nakala mbili za mihtasari ya mkutano wa awali na mkutano anzilishi wa kikundi zilizosainiwa na wanachama wote;

(c) Maazimio ya wanachama kuanzisha na kusajili kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii;

(d) Muundo wa kikundi uliopendekezwa na majina ya viongozi waliopendekezwa;

(e) Orodha ya wanachama wa awali na uthibitisho wa malipo ya michango ya uanachama; na

(f) barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Serikali ya Mtaa au kijiji.

3. Anuani ya kikundi au eneo la kufanyia biashara ya huduma ndogo za fedha;
4. Tunatamka pia kwamba taarifa tulizozitoa hapo juu ikiwemo viambatisho ni sahihi, kwa kadri ya uelewa na imani zetu.

| JINA LA MWANAKIKUNDI | SAINI |
|---|---|
| 1. ……………………...…………........ | ……………...…….………... |
| 2. ……………………...………..……. | ……………...……..……... |
| 3. …………………...……....…………. | ……………...…….………... |
| 4. ……………………………………. | ……………………………. |

Fomu Na.3

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BENKI KUU YA TANZANIA/MAMLAKA KASIMISHWA

HATI YA USAJILI

*(Imeandaliwa chini ya kanuni ya 11(3))*

Na. ya Usajili. …………………………….

(MKOA/MSM/MWAKA/NA.)

Hii ni kuthibitisha kwamba Kikundi cha Huduma Ndogo za Fedha cha Kijamii cha *(Jina la Kikundi)*…….………..…………………………………...… kilichopo *(Mtaa / Kijiji)* ……………………….…………. kimesajiliwa baada ya kukidhi masharti yaliyopo chini ya kifungu cha 28 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, 2018.

Tarehe………………mwezi…………………………………………………

……………………………………….

SAINI

JEDWALI LA TATU

*(Limeandaliwa chini ya kanuni ya 21(2))*

TAARIFA ZA MSINGI ZA FEDHA NA MASUALA MENGINE HUSIKA

SEHEMU A: MAELEZO YA KIKUNDI

Jina la Kikundi …………………………………………………………………………..

Namba ya Usajili…………………………………………………………………………

Kijiji/Mtaa……………………………………………………………………………...

Kata ………………………………………………………………………………………

Wilaya ……………………………………………………………………………………….

Mkoa ……………………………………………………………………………………….

Idadi ya Wanachama: ….……….. (Me)……………. (Ke)…………………

SEHEMU B: IDADI YA MIKOPO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA ………………

| | Salio Anzia | Wakati wa Robo Mwaka | Salio Ishia |
|---|---|---|---|
| Idadi ya Mikopo iliyotolewa kwa Wanaume | | | |
| Idadi ya Mikopo iliyotolewa kwa Wanawake | | | |
| Jumla | | | |

SEHEMU C: THAMANI YA MIKOPO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA…………

(Kiasi kwa Sh.)

| | Salio Anzia | Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa Robo Mwaka | Thamani ya Mkopo Uliolipwa wakati wa Robo Mwaka | Salio Ishia |
|---|---|---|---|---|
| Thamani ya Mikopo | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| iliyotolewa kwa Wanaume | | | | |
| Thamani ya Mikopo iliyotolewa kwa Wanawake | | | | |
| Jumla | | | | |

SEHEMU D: MICHANGO YA WANACHAMA, MICHANGO NA MIKOPO YA KIKUNDI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA ………………………

| | Salio Anzia | Wakati wa Robo Mwaka | Salio Ishia |
|---|---|---|---|
| Michango ya Wanachama | | | |
| Michango Mingine | | | |
| Jumla ndogo | | | |
| Mikopo ya kikundi | | | |
| Jumla | | | |

SEHEMU E: TAARIFA YA MAPATO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA……………

| | Salio Anzia | Robo Mwaka | Salio Ishia |
|---|---|---|---|
| Riba itokanayo na mikopo | | | |
| Mapato yatokanayo na shughuli za kiuchumi za kikundi | | | |
| Misaada | | | |
| Jumla ya Mapato | | | |
| Mgawanyo wa ziada | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Matumizi mengine | | | |
| Jumla ya Matumizi | | | |
| Mapato halisi | | | |

Imeandaliwa na………………………………………………………….

(Jina la kiongozi wa kikundi)

Saini………………………………………

Tarehe ……………………………………………….

Dar es Salaam,
………………, 2019

FLORENS LUOGA
*Gavana*